*Dawa Yako*


## Nyumbani

- Piga simu uwasiliane na maduka ya dawa mengi uulize dawa zako ni pesa ngapi — bei zinaweza kutofautiana hata ndani ya kampuni moja ya maduka ya dawa.
- Tafuta mtandaoni upate tovuti zinazotoa mapunguzo ili kulinganisha bei za dawa na utafute kuponi za punguzo mtandaoni.
- Ipigie simu kampuni yako ya bima. Baadhi ya makampuni yatakupa ‘punguzo la likizo’ ili kulipia oda za safari za zaidi ya siku 30.
    - Huenda utahitaji kulipa bei kamili ya dawa yako mapema lakini unaweza kuomba kurejeshewa pesa kwa kujaza fomu ya madai na kuituma kwa kampuni yako ya bima utakaporudi.
- Piga simu kwa ofisi ya daktari wako na umweleze suala lako (kama vile huwezi kupata vidonge vya kutosha au dawa ni ghali mnoa) na uombe wakuagizie dawa mbadala.

Jambo la Kufanya

Ikiwa Dawa Zako za Usafiri

Ni Ghali Mno



# *Ni PESA NGAPI??*

# Ni PESA NGAPI?!?

Jambo La Kufanya Ikiwa Dawa Zako Za Usafiri Ni Ghali Mno



*Ukimwona Daktari Wako*

## Ukimwona Daktari Wako

- Mwambie daktari wako ikiwa unapangia kusafiri nje ya nchi. Mwambie unaenda wapi na utasafiri kwa muda gani. Daktari wako anaweza kukupa taarifa muhimu kuhusu jinsi ya kulinda afya yako, ikiwa ni pamoja na njia za kujilinda wewe na familia yako dhidi ya malaria.
- Ikiwa huna bima au una Medicaid/Medicare, mwambie daktari wako kuwa una wasiwasi kuhusu gharama za dawa na kwamba unahitaji dawa nafuu zaidi.
- Mwombe daktari wako akupe maagizo ya karatasi ikiwa unapanga kutafuta karibu upate bei nzuri ya dawa yako.
- Muulize daktari wako kama ana mawazo yoyote kuhusu jinsi ya kupunguza bei ya dawa yako.



*Kwenye Duka la Dawa*

## Kwenye Duka la Dawa

- Muulize muuzaji dawa kama anaweza kukupa dawa ya aina ya kawaida au ya bei nafuu.
- Muulize muuzaji dawakama anajua kuhusu kadi za mapunguzo au vocha za dawa unayonunua.
- Mwombe muuzaji dawa apige kwa simu ofisi ya daktari wako ili kuibadilisha akupe dawa ya bei nafuu zaidi.
- Ikiwa maagizo yalitumwa kwa duka la dawa kwa njia ya kielektroniki, waombe watume maagizo hayo ya dawa kwenye duka lingine ikiwa utapata bei nafuu zaidi.


651-201-5414
www.health.state.mn.us
9/2021

DEPARTMENT OF HEALTH

UNIVERSITY OF MINNESOTA